HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe
Baraza la Madiwani,
Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.
MWANZA

YAH: TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA ROBO YA TATU (JANUARI – MACHI) TAREHE 30/04/2018 MWAKA WA FEDHA 2017/2018

1.0. UTANGULIZI

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa taarifa ya matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila robo ya mwaka.

Hivyo taarifa hii itagusa maeneo yafuatayo:-

i. *Taarifa ya chanjo ya watoto wenye umri wa miaka 14 dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi .*
ii. *Taarifa ya ujio wa wadau wa maendeleo kutoka nchi ya Canada*
iii. *Taarifa ya mitihani ya kidato cha Tano mwaka 2018*
iv. *Taarifa ya uhamisho wa Walimu kutoka Idara ya Elimu Sekondari kwenda Idara ya Elimu Msingi*
v. *Taarifa ya uhakiki wa watumishi*
vi. *Taarifa ya Tahadhali ya Utapeli katika Ardhi*

vii. *Taarifa ya Halmashauri kupata hati safi katika hesabu za mwisho kwa mwaka 2016/2017*

viii. *Taarifa ya Maendeleo ya Mradi wa TSCP*

ix. *Taarifa ya kuanza kwa jengo Mako Makuu ya Halmashauri*

x. *Taarifa ya miradi ya maji inayotekelezwa na MWAUWASA*

2.0. UFAFANUZI WA TAARIFA

2.1 *Taarifa ya chanjo ya watoto wenye umri wa miaka 14 dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi .*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuzuia na kuwakinga watoto wa kike dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi, Halmashauri yetu imeanza kutoa chanjo tangu tarehe 23/4/2018 kwa watoto walioko shuleni na mitaani waliozaliwa mwaka 2004 ambao idadi yao ni 2898. Chanjo hii itakuwa ni Endelevu na itatolewa kwenye vituo vyote vinavyotoa huduma za afya na kila mtoto atatakiwa kurudia chanjo hiyo mara baada ya miezi sita. Aidha, Wasichana wenye umri wa miaka 14 ndio watahusika. Wahudumu na waalimu wameshapata mafunzo kuhusu utoaji wa chanjo hii.

2.2 *Taarifa ya ujio wa wadau wa maendeleo kutoka nchi ya Canada*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwezi Machi na Aprili kwa vipindi tofauti Halmashauri ilipokea wageni ambao ni wadau wa maendeleo kutoka nchi Canada. Wageni hawa ni waalikwa Mtaa wa Lukobe ulioko kata ya Kahama. Aidha, kutokana na ushirikiano wa wadau hawa, Mheshimiwa Mbunge na viongozi na wananchi wa Mtaa wa Lukobe, wamekubali kutoa msaada wa ujenzi wa zahanati ya Mtaa ambapo halmashauri imechangia upauaji wa jengo la zahanati na mfadhili amejenga boma na atafanya ukamilishaji na uwekaji vifaa tiba. Pia, wafadhili hawa pia wamekubali kuipatia Halmashauri vifaa tiba kwa matumizi ya zahanati zote ambapo Halmashauri itachangia gharama ya usafiri kutoka nchini CANADA

2.3 *Taarifa ya mitihani ya kidato cha Tano mwaka 2018*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Baraza lako kuwa, Mnamo tarehe 7 - 24/05/2018, kutakuwa na zoezi la mitihani kwa wanafunzi wa kidato

cha sita katika Halmashauri yetu katika shule 5 za sekondari za Bwiru wavulana, Bwiru Wasichana, Taqwa, Rorya na Nyasaka Islamic. Natoa rai kwa viongozi katika ngazi zote kutoa ushirikiano wakati wa zoezi hilo

2.4 *Taarifa ya uhamisho wa Walimu kutoka Idara ya Elimu Sekondari kwenda Idara ya Elimu Msingi*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha robo ya tatu ya Januari – Machi 2018, Halmashauri ilipokea maelekezo kutoka Serikali Kuu juu ya kuwahamisha walimu wa ziada walipo katika shule za sekondari kwenda katika shule za msingi ili kupunguza upungufu wa walimu katika Sekta ya elimu msingi. Hivyo, kufuatia maekelezo hayo, Halmashauri imetekeleza kwa kuwahamisha walimu 36 wa masomo ya Sanaa. Aidha, walimu wote waliohamishwa wamelipwa stahili zao za uhamisho.

2.5 Taarifa ya uhakiki wa watumishi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea na uhakiki wa vyeti vya kitaaluma kwa watumishi wote waliohakikiwa awali na ambao hawakuhakikiwa kwa sababu mbalimbali. Jumla ya watumishi **13** walibainika kutokuwa na sifa za kuendelea na utumishi kutokana na kutokidhi matakwa ya kimuundo.Watumishi hawa wana elimu ya darasa la saba na walijisali kama kidato cha nne. Hivyo, nalitaarifu Baraza lako kuwa, watumishi hawa wamaeondolewa katika utumishi wa Umma na katika orodha ya malipo ya Mishahara ya Serikali.

Pia. Serikali iliagiza kuwaondoa katika orodha ya malipo ya mishahara wa Serikali watumishi wote/watendaji wa Kata na Mitaa walioajiriwa baada ya tarehe 20/05/2004. Hivyo, napenda kuwataarifu kuwa, Halmashauri haikubainika na dosari ya kiutendaji katika uhakiki wa watumishi na watendaji wa Kata na Mitaa walioajiriwa baada ya tarehe 20/05/2004 kwani ilizingatia vema maelekezo ya Serikali yaliyokuwa yametolewa.

2.6 Taarifa ya Tahadhali ya Utapeli katika Ardhi

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, kuna wimbi la matapeli katika sekta ya Ardhi na Mipango Miji hususani katika mazoezi ya mauziano ya viwanja. Kwa mfano katika kipindi miezi mitatu iliyopita, tumeweza kuwakamata matapeli watatu na mashauri yao yamefikishwa katika

Ofisi za RPC. Hivyo, napenda kutoa rai kwa wajumbe wa Baraza hili kuzingatia mambo yafuatayo katika maneo ya kata na Mitaa;

(i) Kuwatangazia wananchi wasinunue kiwanja chochote bila kupata ushauri kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri

(ii) Wananchi watakaokuwa wakihamisha miliki kupitia Ofisi ya Mkurugenzi ni vema wakafika wao wenyewe au wapewe mamlaka ya kisheria (Registered power of attorney) kutoka kwa wamiliki wa ardhi. Kwa wenye shida ya ziada, wafike Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa

(iii) Tunaomba taarifa hizi zitolewe kwenye mitaa yote ili wananchi wajiepushe na matapeli kuwaingiza katika hasara na migogoro isiyo ya lazima.

2.7 Taarifa ya Halmashauri kupata hati safi katika Hesabu za Mwisho kwa Mwaka 2016/2017

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchua fursa hii kulitaarifu Baraza lako la Madiwani kuwa, Katika ukaguzi uliofanywa na mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri imepata **Hati Safi.** Hivyo, Halmashauri imekuwa na mafanikio makubwa katika eneo hili kwani imeweza kupata hati safi kwa miaka mitano mfululizo yaani 2012/2013 hadi 2016/2017. Mafanikio haya yanatokana na ushirikiano, uadilifu na uwajibikaji wa pamoja baina ya Waheshimiwa Madiwani na watendaji katika ngazi zote. Rai yangu ni kuwa juhudi zaidi zitaongezwa katika ushirikiano, udilifu na uwajibikaji ili kuweza kuendelea kuyalinda mafanikio haya.

2.8 Taarifa ya Maendeleo ya Mradi wa TSCP

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa 2015, Halmashauri ya Manispaa katika mwaka wa Fedha 2017/2018, imepanga kujenga barabara ya lami kutoka Buswelu – Kiseke – sabasaba, Makongoro Junction – Mwaloni na Mji Mwema – Isamilo zenye urefu wa kilomita 12.1 . Napenda kulijulisha Baraza hili kuwa, kazi itaanza Mwezi Mei 2018. Mpaka sasa Halmashauri kwa kushirikiana na

Benki ya Dunia imeshapata Kampuni ya Ushauri wa Mradi ya NIMETA Consult yenye Makao Makuu Jijini Dar Es Salaam.

Aidha, kwa sasa Halmashauri iko kwenye hatua za mwisho za mchakato wa kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi na pindi atakapopatikana kwa utaratibu uliopo mtajulishwa. Vilevile, wanachi katika maeneo ambako barabara Buswelu – Kiseke - Sabasaba inapita ulipaji fidia uko hatua za mwisho ambapo jumla ya wananchi 26 Wamelipwa fidia na fedha kiasi cha **Tshs 351,195,480** kimelipwa

2.9 Taarifa ya kuanza kwa jengo Mako Makuu ya Halmashauri

Halmashauri imepokea fedha kwa vipindi tofauti ambapo jumla ya Tshs. 1,050,000,000 ikiwa Tshs 750,000,000 kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na Tshs. 300,000,000 kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Makao Mkuu ya Halmashauri.

Kwa muda mrefu, halmashauri imekuwa na mawasiliano na Wakala wa Majengo Tanzania. hivyo, nachukua fusa hii kulijulisha Baraza lako la Mdiwani kuwa, Wakala wa Majengo Tanzania tayari amenza kazi na anatarajia kukamilisha ifikapo Mwezi Mei 2019. Ujenzi huo utagharimu kiasi cha **Tshs. 3,833,822,825.45**.

Kulingana na gharama za ujenzi kwa mujibu wa mkataba yaani Tshs **3,833,822,825.45,** Halmashauri itapungukiwa kiasi cha **Tshs 2,783,822,825.25** ili kukamilisha ujenzi huo. Fedha hizi zilizopungua zimeombwa kwenye Mpango na Bajeti ya 2018/2019 ili kuweza kukamilisha jengo hilo.

2.10 Taarifa ya miradi ya maji inayotekelezwa kwa kushirikiana na MWAUWASA

Katika Mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri imeendelea kutekeleza miradi ya maji kwa kushirikiana na Mamlaka ya maji MWAUWASA ambapo mpaka sasa miradi ifuatayo imetekelezwa na mingine inatarajiwa kutekelezwa kwa maeneo yafuatayo;

1. Ujenzi wa tanki lenye ujazo wa mita za ujazo 500, mabomba yenye urefu wa mita 11,640 na uwekaji wa pampu ya booster katika maeneo ya Ibanda juu, Ibanda ziwani, Ibanda Busisi, Mihama, na Jiwe Kuu. Jumla ya wanufaika 336 wataunganishwa bure.

2. Ujenzi wa tanki lenye ujazo wa mita za ujazo 1200, mabomba yenye urefu wa mita 20,530 na uwekaji wa pampu ya booster katika maeneo ya Nyasaka, Nsumba, Kiseke, Nundu, Buhilya, Kangae Kaskazini. Jumla ya wanufaika 632 wataunganishwa bure.
3. Ujenzi wa tanki lenye ujazo wa mita za ujazo 1200, mabomba yenye urefu wa mita 9,450 na uwekaji wa pampu ya booster katika maeneo ya Kiloleli B, Nyamanoro Mashariki na Kilimahewa. Jumla ya wanufaika 1,065 wataunganishwa bure.
4. Kubadilisha mabomba katika maeneo ya Kirumba yenye urefu wa mita 8,280
5. Kujenga chanzo kipya cha maji katika eneo la Sangabuye chenye uwezo wa kuzalisha maji kwa siku lita za ujazo 40,000,000 (40,000m3/kwa siku). Maeneo yatakayonufaika ni; Sangabuye, Igombe, Bugogwa, Kabusungu na Buswelu. Mpaka sasa mradi huu uko katika hatua za mwisho za usanifu.
6. Ujezi wa Bwawa la Maji taka lenye uwezo wa lita za ujazo 12,500 kwa siku katika maeneo ya Buswelu, Nyamhongolo ambapo kazi hii bado haijatekelezwa.
7. Kuongeza mtandao wa maji taka mita 843 katika eneo la kilimahewa bigbite, Msuka na Mji Mwema umekamilika.
8. Kubadili mabomba ya maji taka, ujenzi wa chujio la uchafu katika eneo, na ufungaji wa pampu za maji 3 katika eneo la Kirumba kazi hii imefanyika
9. Kujenga mfumo wa kuondoa maji taka katika maeneo ya milimani wenye urefu wa mita 1,750 na jumla ya nyumba 1000 zimeunganishwa katika maeneo ya Kilimahewa A& B
10. Kujenga vyoo katika shule za msingi za Sima, Kiatangiri C, Bondeni, Kilimahewa, Nundu A, Gedeli, Nundu D, Ziwani, Bulola, Kitangiri A, Pasiansi na Buswelu - kazi hii imekamilika
11. Kujenga vyoo katika maeneo ya soko na Nyakato National, Zahanati ya Nyakato, Soko la Buswelu na zahanati ya Nyerere – Kazi hii imekamilika

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa
ILEMELA